



## Karibu kwenye Maktaba!

Nchini Marekani, maktaba yapo kwa sababu tumejitolea kuhakikisha kwamba kila mtu anayeishi hapa anaweza kusoma, kujifunza na kuchanganua maelezo ili kumsaidia kuboresha maisha yake. Maktaba ni jengo ambalo lina vitabu, filamu, muziki na vitu vingine ambavyo mtu ye yote aliye na kadi ya maktaba anaweza kuazima, aende navyo nyumbani ili kutumia, kisha avirudishe maktabani. Uki azima kitu halafu usikirudishe, itakulazimu kuilipa maktaba kitabu, filamu au muziki husika. Ilmradi umerejesha kitu ulichoazima, hatatozwa chochote.

### Pata Kadi ya Maktaba

Kila mtu anafaa kuwa na kadi ya maktaba ili kuazima vitu kutoka maktabani. Ili kupata kadi ya maktaba, unatakiwa kuleta kitambulisho chako chenye picha na hati au barua iliyo na anwani ya mahali unakoishi sasa. Kitambulisho hicho kinaweza kuwa leseni ya udereva au isiyo ya udereva, kadi yako ya kuajiriwa, bili ya matumizi nyumbani, hati za kukodisha nyumba au za kusafiri.

Unaweza kuwa na mtu wa kukusaidia katika mchakato huu ikiwa unahitaji, au mhudumu wa maktaba (mkutubi) anaweza kumwita mkalimani akusaidie. Baada ya hapo mfanyakazi wa maktaba atakupa kadi. Taarifa kukuhusu na aina ya vitu unavyoazima hazitaonyeshwa mtu mwininge ye yote. Hakikisha kuwa unaweka kadi hii mahali salama na usimruhusu mtu mwininge aitumie.

Watoto wako wanaweza kupata kadi yao ya maktaba pia! Wanachohitaji ni mzazi kusaini fomu kwa niaba yao tu.

### Kutoka na Vitu

Utatumia kadi yako ya maktaba ili kuazima vitu kutoka maktabani. Mchakato huo unaitwa kutoka na vitu.

Baadhi ya matawi yana mashine ambayo hukuwezesha kujiondolea vitu mwenyewe. Unaweza pia kuchagua lugha unayopendelea ili stakabadhi ya kutoa vitu ichapishwe katika lugha hiyo. Stakabadhi hiyo hukuonyesha vitu unavyoodoa maktabani na wakati unapotakiwa kuvirudisha.

Huwa kuna wafanyakazi wa maktaba walio tayari kukusaidia katika tawi lolote.

## **Huduma na Mipango**

### **• Watoto na Vijana**

- Maktaba ni mahali pazuri pa kuwaleta watoto wako, kutoka wale wachanga kabisa hadi walio shule ya upili! Wanaweza kuangalia vitabu katika Kiingereza na lugha nyingine, vikiwemo vitabu vya kurasa ngumu kwa ajili ya wachanga na CD za muziki na filamu kwa wakubwa. Matawi mengi hata yana toi unazoweza kuondoka nazo maktabani. Wafanyakazi wa maktaba huwakaribisha watoto na vijana kuja kujifunza, kutangamana na marafiki au kusoma tu.
- Maktaba pia ina shughuli za kufurahisha kwa watoto wa umri wote. Watoto wadogo wanaweza kwenda sehemu ya masimulizi ya hadithi pamoja na bibi/nyanya au mndugu mwingine; watoto wako wanaoenda shule wanaweza kufurahia vipindi kuhusu sayansi, wanyama na sanaa! Waulize wafanyakazi wa maktaba wakupe shajara ya muda wa hadithi na vipindi.

### **• Watu wazima**

- Maktaba hutoa huduma nyingi kwa watu wazima jinsi tu ilivyo kwa watoto. Kuna vitabu vya Kiingereza na lugha nyinginez, filamu na muziki, vyote unavyoweza kutoka navyo, pamoja na huduma nyingi za elektroniki unazoweza kutumia kadi yako ya maktaba kufikia bila kutembelea jengo la maktaba. Watu wazima pia wanakaribishwa kuja kujifunza, kutangamana na marafiki, kutumia kompyuta au kusoma tu. Maktaba pia ina miradi mbalimbali kwa ajili ya watu wazima! Waulize wafanyakazi wa maktaba wakupe shajara ya miradi hiyo.

### **• Kompyuta na Wi-Fi**

- Matawi yote ya maktaba na Maktaba Zinazohamishika zina Wi-Fi ya bure. Upo huru kutumia kompyuta katika tawi lolote la maktaba ukiwa na kadi yako ya maktaba. Ikiwa umesahau kadi yako ya maktaba, waulize wafanyakazi wa maktaba wakusaidie.
- Ikiwa huna uzoefu mwingi wa kutumia kompyuta, unawenza kujifunza jinsi ya kutumia katika mradi wa maktaba ukiwa na wafanyakazi wetu. Wafanyakazi wa maktaba wanaweza kukupa ratiba.

### **• Kuna Mkalimani**

- Wafanyakazi wa maktaba hutaka kufanya muda unaotumia maktabani uwe mwema na wenyе manufaa. Ikiwa unahisi ni vizuri zaidi kuzungumza na mkalimani ili kuuliza maswali na kupata maelezo, tafadhali waombe wafanyakazi wa maktaba wakuitie.

## **Jifunze Kiingereza**

Mango Languages ni mfumo rahisi na wa kufurahisha wa kujifunza Kiingereza. Unawenza kuutumia bure ukiwa na kadi yako ya maktaba.

Jaribu kuufikia kwa kwenda kwenye [thelibrary.org/mango](http://thelibrary.org/mango). Unaweza kuanza kujifunza mara kwa mara kwa kuchagua Ufikiaji wa Wageni (Guest Access) au unaweza kuunda nenosiri ili kila wakati unaporudi kwenye ukurasa, uweze kuendelea kutoka ulipoachia.

**Karibu kwenye maktaba yetu!**  
**Tunatumai kwamba utatutembelea mara nyingi na kujisikia huru**  
**kuwauliza wafanyakazi wetu kuhusu huduma zetu zote.**

*Mradi huu unasaidiwa na Taasisi ya Makumbusho na Huduma za Maktaba kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Maktaba na Teknolojia inayoendeshwa na Maktaba ya Jimbo la Missouri, ambayo ni idara ya Waziri wa Nchi na Marafiki wa Maktaba.*